THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/1 **KISWAHILI 1**

*(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)*

*Muda: Saa 3* *Jumatatu 11 Februari 2008 mchana*

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali matano (5) kwa kuchagua swali moja kutoka kila sehemu.
3. Simu za mkononi haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
4. **Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.**

Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

### HISTORIA

1. Eleza sababu zinazokushawishi ukubali kuwa chimbuko la Kiswahili siyo Uganda.

2. **Kukua na kuenea kwa Kiswahili kunachangia kufa kwa lugha za asili. Jadili kauli hii kwa kutoa mifano hai.**

3. Eleza uhusiano uliokuwepo kati ya Kamati ya Lugha ya Kiswahili na Taasisi ya Ukuzaji Kiswahili.

## SEHEMU B (alama 20)

### SARUFI

4. Tunga sentensi sahili na changamano kisha zichanganue sentensi hizo, moja kwa njia ya matawi na nyingine kwa njia ya jedwali. Uchanganuzi uzingatie hatua **tano (5)**.

5. Nomino zikiwekwa katika ngeli kwa kufuata kigezo cha upatanisho wa kisarufi zina viambishi viwili, cha umoja na wingi. Jadili kauli hii kwa kutoa mifano ya nomino **tano (5)** kuthibitisha msimamo wako.

6. Onesha tofauti ya kivumishi na kielezi. Toa ufafanuzi kwa kutumia aina **nne (4)** za vivumishi na aina **nne (4)** za vielezi.

## SEHEMU C (alama 20)

### MATUMIZI

7. Utata huweza kusababishwa na mnyumbuliko wa vitenzi. Thibitisha kauli hii kwa kutumia mifano **mitano (5)** ya mnyumbuliko wa vitenzi tofauti.

8. (a) Eleza maana ya umahiri wa lugha.

   (b) Fafanua changamoto **nne (4)** zinazoukabili umahiri wa lugha.

9. Kwa kutoa mifano **mitano (5)** eleza uhai wa lugha.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (alama 20)

## UTUNGAJI

10. Andika insha ya maneno yasiyozidi 400 na yasiyopungua 350 kuhusu faida na hasara za biashara huria.

11. Ni mambo gani muhimu ya kuzingatia wakati wa kutayarisha kadi ya mwaliko? Andika kadi ya mwaliko kuthibitisha mambo uliyoyataja.

12. Andika taarifa ya kutuma gazetini kuhusu kupotelewa na ndugu yako.

## SEHEMU E (alama 20)

## UFAHAMU

13. Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Maisha yamejaa **pingamizi** mbalimbali. Siti angaliwezaje kufaulu kama asingalijaribu kuzishinda kama alivyotenda!

Hadithi ya Siti, binti wa baba mkulima na mama mfinyanzi ambao hawakujua kitu kingine chochote katika dunia isipokuwa dhiki chungu na umaskini mkali, ilianza kuandikwa baada ya miaka miwili ya mauti yake. Kama haisadikiki sasa kama hadithi yoyote katika Alfu-lela-ulela ilivyo, sababu yake ni kwamba alionyesha uwezo na bidii kubwa sana kuliko ilivyotazamiwa katika maisha yake.

Aliishi maisha ya kukumbukwa milele juu ya pingamizi zake za ujinga wa kusoma, umaskini na unyonge. Hili lilikuwa jambo kubwa sana kwa mwanamke wa cheo chake. Alionyesha **johari** iliyowezekana kupatikana kwa mwanamke kama mila iliyomnyima ushirika iliwezekana **kuhidiwa**. Wazo la kuhidi maisha yake katika mji lilikuwa moja katika **zinduna** kubwa katika alizopata kugundua katika dunia hii. Kama nuru ya wazo hili isingelimulika katika moyo wake, au kama angalifaitika kutumia nuru hii upesi kama ilivyowezekana, maisha yake yote yangaliishia katika miaka ya sahau, umaskini wa dhiki; angaliona kwamba ilikuwa watu wengine siku zote, si yeye mwenyewe, waliokuwa wakipata fedha, ustawi, anasa na wingi wa faraja za maisha. Hili lilikuwa kweli, kweli tupu kwa kadri wasifu wake uliojaa mishuko ya tope na mainuko ya ajabu unavyojieleza wenyewe kwa watu.

Siti alikuwa si mmoja wa wahuni waliozoea kutoroka kwao wakakimbilia katika miji kukaa kama **chaza** juu ya mwamba; au kama **kupe** na mkia wa ng'ombe. Uzuri wa majengo mbalimbali ya mji mkuu wa kisiwa cha Unguja, pamoja na mchanganyiko wake wa ajabu wa lugha vilikuwa si vitu vya mvuto wowote juu yake. Hakutaka kuwa **kimelea** cha mji. Alikuja mjini na kusudi maalum.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Alitamani kufanya kazi pale. Na kama watu wote waliokuwa na akili njema, hakupenda ustawi wake utokane na mapendeleo yoyote. Alitaka utokane na ustahili wake mwenyewe. Mahali alipochagua kutenda tendo hili kubwa palikuwa hapa mjini. Mahali pengine popote palikuwa hapafai kwa tendo kama hili.

**MASWALI**

(a) Andika kichwa cha habari hii.

(b) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mistari.

(c) Mwandishi ana maana gani anaposema "kama an_alifaitika kutumia nuru hii upesi kama ilivyowezekana maisha yake yote yangaliishia katika miaka ya sahau, umaskini na dhiki"

(d) Wazazi wa Siti walikuwa wanafanya kazi gani?

(e) Kwa mujibu wa habari hii Siti yu hai ama amefariki?

(f) Eleza kwa mistari miwili maisha ya wazazi wake Siti.

(g) Unadhani kwa nini Siti [illegible]?

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org